JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)

MKOA WA KIGOMA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU

KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI

CHA TAREHE 23/08/2017 KATIKA UKUMBI WA

HALMASHAURI WILAYA YA KASULU

Imeandaliwa Na:

Ofisiya Mkurugenzi Mtendaji

HalmashauriyaWilaya

S. L. P 97

KASULU.

AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 23/08/2017

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda za Mkutano wa Baraza la Madiwani **23/08/2017**
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano wa tarehe **28/04/2017**
4. Kupokea taarifa toka kwa Wenyeviti wa Kamati.
    - Taarifa ya kamati ya fedha Uongozi na Mipango kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017.
    - Taarifa ya kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017.
    - Taarifa ya kamati ya Huduma za Jamii kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017.
    - Taarifa ya kamati ya kudhibiti Ukimwi kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017.
5. Kumchagua makamu Mwenyekiti na kuunda kamati kwa mwaka 2017/2018
6. Kufunga Kikao

MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 23/08/2017 ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI (W) KASULU.

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

NA	JINA	KATA	CHEO
1	Mhe: Yohana.P.Mshita	Diwani Kata Nyakitonto	Mwenyekiti H/W
2	Eng.Godfrey Kasekenya	Mkurugenzi Mtendaji	Katibu
3	Mhe: Saidi R.Ndiyunze	Diwani kata ya Muzye	Mjumbe
4	Mhe;Banka J.Balagulana	Diwani Kata HeruUshingo	Mjumbe
5	Mhe: Anna T.Mwanandota	Diwani Kata Nyamnyusi	Mjumbe
6	Mhe: Gody L.Nkulizo	Diwani Kata Kurugongo	Mjumbe
7	Mhe: Hilda B.Lusaka	Diwani Viti Maalum	Mjumbe
8	Mhe.Fidel E.Mtemwa	Diwani Kata ya Bugaga	Mjumbe
9	Mhe: Rebeka Dangudangu	Diwani Viti Maalum	Mjumbe
10	Mhe: Agnes Kanyamangenge	Diwani Viti Maalum	Mjumbe
11	Mhe:Ammando Ndondeye	Diwani Kata Nyamidaho	Mjumbe
12	Mhe:William Luturi	Diwani Kata Nyachenda	Mjumbe
13	Mhe:Mwasi Mchunga	Diwani Viti Maalum	Mjumbe
14	Mhe:Monica Mayoba	Diwani Viti Maalum	Mjumbe
15	Mhe:Hamenyimana Gutabaga	Diwani Kata ya Kigembe	Mjumbe
16	Mhe:Renatha Mizungo	Diwani Viti Maalum	Mjumbe
17	Mhe:Ezekiel K. Mshingo	Diwani Kata Kagera Nkanda	Mjumbe
18	Mhe:Eliya C. Kagoma	Diwani Kata ya Kitanga	Mjumbe
19	Mhe:Belisia Solomon	Diwani Kata ya Kalela	Mjumbe
20	Mhe:Skola Mpawe	Diwani Viti Maalum	Mjumbe
21	Mhe:Sabas Matabura	Diwani Kata ya Kitagata	Mjumbe
22	Mhe:Fredrick H. Nyamwombo	Diwani Kata ya Buhoro	Mjumbe
23	Mhe:Moris F. Changuvu	Diwani Kata Shughuliba	Mjumbe
24	Mhe:Abel Jonas Kaja	Diwani Kata RungweMpya	Mjumbe
25	Mhe:Fabiano Doragi	Diwani Kata ya Rusesa	Mjumbe
26	Mhe:Baraka C. Mkuyu	Diwani Kata ya Kwaga	Mjumbe
27	Mhe:Mbiha N.Issaya	Diwani Kata ya Titye	Mjumbe
28	Mhe:Elias Y,Masende	Diwani Asante Nyerere	Mjumbe
29	Mh:Poteza L.Kilali	Diwani Kata ya Makere	Mjumbe
30	Mhe:Asia Kasebo	Diwani Viti Maalum	Mjumbe

WAJUMBE WASIOHUDHURIA

NA	JINA	JIMBO	SABABU
1	Mhe: Agustine Hole Vuma	Mbunge jimbo la Kasulu [V]	Kwa taarifa

ORODHA YA WATAALAM

NA	JINA	CHEO
1.	Bw.Tumsifu Kiwoli	Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi (w)
2.	Bw: Jeconiah J.N	Mkuu wa Idara Mifugo na Uvuvi (w).
3.	Bw: Simon Kichumu	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
4.	Bw.Mikidadi Mbaruku	Kaimu Mkuu wa Idara ya Maji(w)
5.	Bi. Bertha Bikulamuchi	Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii (w)
6.	Bw. Amandus Nzamba	Afisa Tarafa Heru Chini
7.	Bw.Elisha Nayingo	Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi (w)
8.	Bw: Obed Chigera	Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira(w)
9.	Bw; Kilatu J.W	Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu&Ufuatiliaji (w)
10.	Bw. Amede E.A	Mweka Hazina (w)
11.	Bw; Gideon Katulumla	Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
12.	Bw :Alex L. Wambura	Afisa Tarafa Makere
13.	Bw. Thomas Magambo	Kaimu Afisa Tarafa Buyonga
14.	Bi. Leocadia Chunya	Kaimu Afisa Tarafa Buhoro
15.	Bw. Mohamed Omary	Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili
16.	Bw.Ezekiel Badeleya	Kaimu Afisa Manunuzi
17.	Dr. Florian Tinuga	Mkuu wa Idara ya Afya
18.	Bw Emmanuel Ladislaus	Mkuu wa kitengo cha Sheria
19.	Bw.Nicholaus Edward	Kaimu Afisa Elimu Msingi
20.	Bw. Muguha T. Muguha	DAS Kasulu
21.	CPA Festo Kuzengwa	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani
22	Bw.Simon Ntinda	Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika
23	Bw. Ernest Msonge	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA

VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA

NA	JINA	CHEO
1	Bw:Ezekiel Kaloba	Mwenyekiti CCM (W)
2	Bw;Nabothi Manyonyi	Katibu CCM (W)
3	Bw;Hitlet Y.Hitlet	Mwenyekiti NCCR - Mageuzi
4	Bw:Danford Kagabo	Katibu NCCR - Mageuzi
5	Bw:Emanuel S. Ninkuli	Katibu CDM(W)

WAGENI WAALIKWA

NA	JINA	CHEO
1	Sospeter Kungura	Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kasulu
2	Audax Karurama	CM Muyowosi
3	Moses D.Msuluzya	AAS[LGM]
4	Juvenary Leonard	DBC
5	SS Amir Mvumbagu	Kaimu Mshauri wa Mgambo

WAANDISHI WA HABARI

NA	JINA	CHEO
1	Bw:Respice Swetu	Mwandishi Majira
2	Bw:Albert Kavano	Radio Kwizera
3	Bw:Saidi Juma Said	Chanel Ten
4	Bi:Magreth Magoso	Jamboleo
5	Bw:Audax Ignas	TBC 1
6	Bw:Kadeslaus Simon	Mwananchi

VIONGOZI WA MADHEHEBU

NA	JINA KAMILI	DHEHEBU
1	Mch. Juma Mathayo Juma	AICT
2	Mch.Elias Majoh	KKKT
3	Mch.Simon Bakunda	EAGT
4	Mch.Isaka Yumvila	ANGLIKANA
5	Mch.Japhari Iddi	SHIA

HWK/BM/AG/ NA/21/2016/2017 -KUFUNGUA MKUTANO

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti baada ya kuona akidi ya Wajumbe inatosha Kufungua kikao.

Mwenyekiti alianza kusoma Dua la kuliombea Baraza la Madiwani.Baada ya kusoma Dua Mwenyekiti alifungua Mkutano saa **04.35** Asubuhi.

Katibu alitoa nafasi ya Wajumbe kuuliza maswali ya papo kwa papo kwa kufuata orodha iliyoandaliwa.

MASWALI YA HAPO KWA HAPO.

Mheshimiwa Fredrick Nyamwombo.

Kuhusu utafiti wa Zao la Kahawa na Ngano uliofanyika mwaka 2013/2014.Je ni lini Serikali itatoa mrejesho wa utafiti huo katika Kata ya Buhoro?

Ilifafanuliwa kuwa;- Taratibu za tafiti za zao la Kahawa na Ngano bado zinaendelea katika Kata ya Buhoro na matokeo ya awali yanapatikana Idara ya Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika.

Mheshimiwa Jonas Abel Kaja
Tarehe 21/07/2017 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania DKT John P.J.Magufuli alifanya ziara katika Wilaya ya Kasulu na kuruhusu wananchi kulima ndani ya eneo la hifadhi ya misitu Kagerankanda kwa mashamba ya zamani bila kuanzisha mashamba mapya. Je kwanini wananchi wanaendelea kupigwa na kunyang'anywa mali zao katika eneo la Msitu la Mkuti Kaskazini?

Ilifafanuliwa kuwa maeneo yote ya hifadhi yanatakiwa kulindwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Amando A.Ndondeye
Ardhi inamilikiwa na Kijiji Serikali inapohitaji ardhi lazima iombe Kijiji,Je zoezi la usajili wa Mifugo,uwekaji chapa na utatuzi wa migogoro ya wakulima na wafugaji lini itapata ufumbuzi?

Ilifafanuliwa kuwa zoezi la usajili wa mifugo utaenda sambamba na uwekaji wa chapa hii itatusaidia kufahamu idadi halisi ya mifugo na kuweza kutenga maeneo ya malisho na hiyo itasaidia kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji.

SALAMU ZA SERIKALI
Salaam za Serikali zilitolewa na Katibu Tawala wa Wilaya kwa niaba ya Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kasulu.Kumekuwa na tabia ya ukiukwaji wa kanuni, Sheria na Taratibu za nchi.

- Kumekuwa na tabia ya kutenga wananchi wenzao katika vijiji kufanya hivyo ni mpaka maelekezo ya Mahakama tu na si vinginevyo.Kumekuwepo na tabia ya kuchoma nyumba za wananchi,kuchoma mazao na kuua mifugo inapobainika mwananchi ana kosa taratibu zifuatwe za kurudisha katika Jamii.
- Migogoro ya Ardhi viongozi wa Seriklali wanachangia sana kuwepo kwa migogoro hiyo na kusababisha kudhorotesha

shughuli za kimaendeleo na kuendeleza mivutano isiyo ya lazima.

- Migogoro ya Jamii kuweka vikwazo kwa wakandarasi wa ujenzi wa barabara,ushauri ni kijiji kutenga eneo la huduma za Jamii.
- Kudhibiti uvamizi wa maeneo maalumu yaliyotengwa yatumike kwa kazi iliyotengwa tu.
- Uingiaji wa mifugo bila kufuata utaratibu unatuharibia mipango yetu ya Kiuchumi [Uwekezaji]
- Wananchi kuuziwa maeneo oevu kinyume kabisa na taratibu wanachi ngazi ya kijiji waache kuuza aeneo oevu ili maeneo hayo yatumike kama yalivyoainishwa katika sheria za Kimataifa.

.

HWK/BM/AG/ NA/22/2016/2017 KUTHIBITISHA AGENDA

Agenda 6 zilithibitishwa kujadiliwa.

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda za Mkutano wa Baraza la Madiwani **23/08/2017**
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano wa tarehe **28/04/2017**
4. Kupokea taarifa toka kwa Wenyeviti wa Kamati.
    - Taarifa ya kamati ya fedha Uongozi na Mipango kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017.
    - Taarifa ya kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017.
    - Taarifa ya kamati ya Huduma za Jamii kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017.
    - Taarifa ya kamati ya kudhibiti Ukimwi kwa kipindi cha Aprili – Juni 2016/2017.
5. Taarifa ya ziara ya kamati ya Fedha katika hifadhi ya Nyamroha.
6. Uchaguzi wa makamu Mwenyekiti na kuunda kamati kwa mwaka 2017/2018
7. Kupitisha ratiba ya vikao vya Halmashauri kwa mwaka 2017/2018,
8. Mengineyo
9. Kufunga Kikao

HWK/BM/AG/ NA/23/2016/2017 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA TAREHE 28/04/2017

Muhtasari uliwasilishwa mkutanoni na kupokelewa katika kujadili yafuatyo yalisisitizwa;-

- Mh.Mbiha N.Issaya ni kati ya wajumbe walioiuliza maswali ya papo kwa papo katika mkutano wa baraza la madiwani robo ya III.
- Wajumbe walisisitiza asilimia za Vijiji na Kata zinazotokana na mapato ya ndani zianze kurudishwa.
- Kuanzisha Vyanzo vipya vya Mapato ikiwa ni pamoja na kuanzisha Soko la pamoja Kandokando ya Mto Malagarasi.
- Mnara wa simu wa Tigo ambapo Kampuni humlipa bwana Fiile Kanogu ufanyike ufuatiliaji na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake ya kuchukua malipo ya pango la mnara wa simu kinyume cha taratibu.
- Wajumbe wa Serikali za Vijiji wapewe mafunzo ili waweze kufahamu majukumu ya utendaji kazi katika maeneo yao.
- Ufanyike ufuatiliaji wa Minara yote ya simu ili waweze kulipa Service Levy.
- Wananchi wote walioingia na kuendesha shughuli ndani ya hifadhi wakamatwe na washitakiwe.
- Hifadhi ya wanyamapori ya Nyamroha ilindwe kwa kutumia sheria mama wakati mchakato wa kutengeza sheria ndogo unaendelea.
- Ufanyike mchakato wa kufanya mawasiliano na Mkurugenzi wa Wilaya ya Buhigwe ili barabara ya Kajana Katundu iliyofungwa tangu mwezi mei 2017 kwa ajili ya ujenzi wa Kalvati iweze kufunguliwa.
- Mkandarasi aliyekuwa anajenga mradi wa umwagiliaji Rungwe mpya aliondoka na madeni ya Vibarua wake.
  Ilifafanuliwa kuwa hatua za kisheria zichukuliwe ili vibarua wanaomdai mkandrasi aweze kuwalipa fedha zao.

HWK/BM/AG/ NA/24/2016/2017 .KUWASILISHA TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ROBO YA IV (APRILI – JUNI 2016/2017)

TAARIFA YA KAMATI FEDHA UONGOZI NA MIPANGO.

Taarifa ya Kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango ziliwasilishwa na kupokelewa,katika kujadili yafuatayo yalisisitizwa;-

- Kuhusiana na mnara wa Tigo uliopo Jengwe, Mnara wa simu wa Tigo ambapo Kampuni humlipa bwana Fiile Kanogu ufanyike ufuatiliaji ili Halmashauri iweze kunufaika na tozo inayotokana na Mnara huo.
- Ilishauriwa kuwa, Halmashauri ione haja ya kuandaa utaratibu wa kutoa mafunzo kwa Viongozi wa Vijiji ili waweze kufahamu taratibu na mbinu zitakazowasaidia kubaini, kusimamia na kutetea Maslahi ya Halmashauri.
- Wajumbe waliazimia kuwa, Wavamizi wote walio katika maeneo ya Hifadhi waondoke mara moja na kusiwe na Mjadala katika suala hilo.Aidha Mwansheria wa Wilaya alishauri kwamba, kwa sasa zitumike Sheria Mama za uhifadhi wa Mazingira katika utekelezwaji wa suala hilo wakati maandalizi ya Sheria ndogo yanafanyika.
- Wajumbe walitaka kujua kuhusu suala la kufutwa kwa hoja;- Ilielezwa kuwa hoja zinazofutwa ni zile zisizo na mashiko.Hoja zote za Kisheria hazitofutwa bali zitaendelea kufuatiliwa kwa kina kadri ya taratiu za kisheria zinavyoongoza.
- Kuhusiana na ombi la mjumbe kutaka kufanyike utaratibu wa sehemu ya mapato kuelekezwa ngazi ya kata kwa ajili ya kusaidia majukumu.;- Ilielezwa kuwa ieleweke kwamba fedha zote zinazokusanywa ni mali ya halmashauribali hivyo wazo hilo lichukuliwe na kupelekwa Kamati ya fedha uongozi na mipango kwa ajili ya kulifanyia mchakato zaidi.

KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII.

Taarifa kamati ya huduma za jamii ziliwasilishwa mkutanoni na kupokelewa, katika kujadili yafuatayo yalisisitizwa:-

- Kuhusu ufaulu wa asilimia 40.6 katika mtihani wa utimilifu mkoa wa Kigoma umetupa picha ya wanafunzi wetu kufanya vizuri katika mtihani wao wa Mwisho[darasa la Vii 2017]
- Ufanyike mchakato wa kuifungua shule ya Sekondari Kitanga iende sambamba na urejeshaji wa madawati 100 yaliyoazimwa na kupelekwa shule ya Sekondari Muyowosi.

KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Taarifa ya kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira iliwasilishwa Mkutanoni na kupokelewa na katika kuijadili yafuatayo yalijitokeza;-

- Kuendelea kwa utatuzi wa Mgogoro wa Mpaka kati ya Kijiji cha Kitagata na Nyachenda.

  Mjumbe alitaka kufahamu,kuhusu Mkandarasi aliyekua anajenga Barabara ya scheme ya scheme ya titye aliyeacha kazi na kuondoka huku akidaiwa na vibarua wake;-

  Ilijibiwa kuwa,utaratibu unafanyika ili kupata mkandarasi mwingine ili aweze kuendelea na kazi.Aidha kama kunauthibitisho wa kudaiwa na vibarua wake upatikane uthibitisho ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

Taarifa ya kamati ya kudhibiti ukimwi iliwasilishwa mkutanoni na kupokelewa .

UWASILISHWAJI WA RASIMU YA SHERIA NDOGO.

Taarifa ya uwasilishwaji Rasimu ya Sheria ndogo iliwasilishwa kikaoni na kupokelewa,katika kuijadili yafuatayo yalijitokeza;-

- Wajumbe walishauri taratibu zifuatwe ili shaeria hizo ziweze kuidhinishwa na kuanza kufanyiwa kazi.

- Wajumbe walitoa ombi;-Kwa kuwa Kata zipo ishirini na moja na baadhi ya Kata hazina watendaji , uandaliwe utaratibu wa kutoa Elimu kwa Wananchi kuhusiana na Sheria ndogo.

HWK/BM/AG/ NA/24/2016/2017 TAARIFA YA ZIARA YA KAMATI YA FEDHA KATIKA HIFADHI YA WANYAPORI KATOTO.

Taarifa ya ziara ya kamati ya Fedha Uongozi na Mipango iliwasilishwa kikaoni ikiwa na Taarifa pamoja na mapendekezo kama ifuatavyo.

Kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango katika Kikao cha tarehe 15/05/2017 kiliazimia kwenda eneo la Kitalu cha uwindaji kuhakiki mpaka wa eneo la Kitalu cha uwindaji cha Katoto pamoja na kuona hali ya uvamizi uliofanyika ndani ya Hifadhi.

Katika ziara hiyo yafuatayo yalionekana;-

1. Wavamizi wameingia ndani ya eneo la hifadhi na kuendesha shughuli za Ufugaji , Kilimo na Makazi kinyume cha taratibu.
2. Ukataji wa miti unafanyika kwa kasi kubwa na kilimo.
3. Eneo la Ardhi **OEVU** linaharibiwa kwa kasi kwa shughuli za Kibinadamu licha ya kuwa chini utunzaji wa maeneo Oevu duniani – RAMSAR ambapo Tanzania iliridhia kuwa mwanachama mwaka 2002,
4. Uvamizi wa shirika la NARCO katika eneo la uwekezaji na ndani ya Ardhi ya Kasulu.
5. Wavamizi kujimilikisha maeneo makubwa yasiyo rasmi ndani ya mipaka ya hifadhi.
6. Kukosekana kwa sheria ndogo ambayo itatumika katika shughuli za uhifadhi pamoja na kuboresha mapato ya Halmashauri .
7. Kutokana na jina la kitalu kutaja Wilaya ya Uvinza [Makere,Uvinza FR-Open Area] mapato ya yanayotokana na hifadhi hugawanywa katika Wilaya mbili Kasulu na Uvinza

ambapo Wilaya ya Uvinza hawana hifadhi.Kamati imependekeza jina la kitalu liitwe Nyamroha FR-Open Area ili kusiwe na mgawanyo wa mapato yanayotokana na hifadhi kwenda wilaya ya Uvinza.

8. Itolewe elimu ya usomaji wa Ramani na kutafsiri ya mpaka kati ya kitalu na Kijiji cha Kagerankanda.
9. Maeneo waliyonunua akina Lukindika na Matatula Majani waliuziwa maeneo hewa ambayo yamo ndani ya eneo la hifadhi.
10. Uvamizi wa eneo la hifadhi limepelekea mwekezaji kushindwa kuweka miundombinu ya kutosha wa ajili ya vivutio vya utalii.
11. Kijiji cha Kagerankanda kukiuka utaratibu wa kugawa ardhi kwa kutoa maeneo ya makazi,Kilimo na Ufugaji ndani ya eneo la uwekezaji.
12. Mpaka wa kiutawala kati ya Wilaya ya Kasulu na Uvinza unaeleweka vizuri kwa kuzingatia GN namba 117 ya mwaka 1980 na Ramani kusababisha mwingiliano wa matumizi ya ardhi.

MAPENDEKEZO YA KAMATI.

1. Mipaka ya hifadhi yote ilindwe bila kupunguza eneo la hifadhi ndani ya wilaya ya Kasulu.
2. Ofisi ya Idara Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji na Idara ya Ardhi na Maliasili wakae na kubainisha vyanzo vingine vya mapato kwa kushirikiana na Mwekezaji.
3. Mwekezaji aalikwe kuhudhuria mkutano ujao wa Baraza la Madiwani.
4. Wafugaji na Wakulima waliomo ndani ya hifadhi wapewe taarifa ya kuodoka mapema na kutoendelea tena kufanya shughuli za kiuchumi ndani ya eneo la hifadhi.
5. Wananchi waliouziwa maeneo ndani ya hifadhi waondoke wote.
6. Eneo la Ardhi Oevu lihifadhiwe kwa kutokuzingatia mipaka ya Kiutawala [Wilaya na Wilaya]

7. Ziwekwe alama za kudumu na zinazoonekana eneo la mipaka ya hifadhi na eneo la mipaka ya kiutawala,Aidha kamati ilikubliana kwamba wataalamu wa Ardhi na Maliasili kwenda mapema kijiji chakagera nkanda kuwaonesha viongozi wakijiji mpaka wa kijiji na hifadhi kwa kufuata ramani ya kijiji ya mwaka 2007 .
8. Kamati ilikubaliana kwa pamoja kwamba wafugaji ndugu Matatula Majani, Ndugu Lukindika,ndugu Mashenene na wengineo ambao wanaishi na kufanya shughuli zao ndani ya hifadhi waondoke kwani eneo wanapofanyia shughuli zao za kiuchumi ni eneo la hifadhi.
9. Ili kulinda eneo la Ardhi OEVU wananchi wa eneo la Katoto wahamie eneo la upande wapili [Kusini] m wa barabara unaotenganisha hifadhi na makazi ya wananchi kwa kuzingatia Kaya za wakazi wenyeji [Watusi]
10. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ifahamishwe kuhusiana na uwekezaji katika kitalu cha uwindaji wa kitalii Nyamroha,ikiwa ni pamoja na kamati husika kwenda eneo la hifadhi ya wanyama pori mapema kabla ya tarehe 15/08/2017 ili kujenga ufahamu wa pamoja wa eneo husika .
11. Itolewe elimu ya uhifadhi wanyama Pori katika vijiji vinavyozunguuka hifadhi ili waweze kuelewa rasilimali iliyopo na kuweza kuitunza.elimu hiyo itolewe kwa kutumia vyombo vya habari pamoja na kamati ya uchumi ujenzi na mazingira.
12. Ufuatiliaji ufanyike kwa kutizama uhalali wa ranchi za mifugo zinazomilikiwa na NARCO Katika eneo la Kasulu.
13. Itafutwe ramani yenye kuonesha mipaka ya kiutawala ya wilaya ya kasulu na uvinza na kubaini mipaka halisi.
14. Uwepo umbali wa wa km 2.5 kutoka eneo la kambi ya uwindaji wa kitalii mpaka eneo la makazi ya watu na shughuli za kibinadamu,hivyo kamati imewataka kaya zilizopo karibu na kambi ya utalii ziondoke hususani Ndugu Kulilo na wenzake.
15. Kwakuwa eneo la kitalu kubaki Wilaya ya Kasulu ,ni vyema eneo hilo kuitwa kwa jina la Nyamroha hunting block ,badala ya Makere ,Uvinza ,FR Open Area.

16. Ipitishwe sheria ndogo haraka ili kuweza kunufaika na mapato yatokana na uvuvi kutoka kwa mwekezaji.
17. Kamati ilikubaliana kwa pamoja kwamba tarehe 15/09/2017 ,mipaka ya hifadhi pamoja na mipaka ya kiutawala iwe imewekwa Alama(Beacon)

KUPITIA RATIBA PENDEKEZWA YA VIKAO.

Wajumbe waliipitia ratiba ya vikao kwa mwaka 2017/2017 na kushauri ifuatavyo;-

- Wah.Madiwani wawe wanapewa taarifa kuhusiana na mabadiliko ya Ratiba za Vikao hususani zinapotokea dharura zisizo zuilika.

HWK/BM/AG/NA/25/2016/2017 UCHAGUZI WA MAKAMU MWENYEKITI NA KUUNDA KAMATI KWA MWAKA 2017/2018.

Uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti unafanyika baada muda wa kukaa madarakani kumalizika na muda wa kupata kiongozi mwingine umewadia ambapo atahudumu kwa mwaka 2017/2018.
Kutokana na vyama kuwa zaidi ya kimoja vyama viwili vilisimamisha wagombea ambao wameainishwa hapa chini;-

Na	Jina Kamili	Chama
1	Saidi R.Ndiyunze	CCM
2	Baraka C.Mkuyu	CHADEMA

Jumla ya wajumbe waliopiga kura walikuwa 27 hakuna kura iliyoharibika.Baada ya kuhesabu kura matokeo yalikuwa kama ifuatavyo;-

Na	Jina Kamili	Chama	Idadi ya Kura
1	Saidi R.Ndiyunze	CCM	20
2	Baraka C.Mkuyu	CHADEMA	7
			27

Msimamizi wa uchaguzi alimtangaza Mheshimiwa Saidi R.Ndiyunze kutoka Chama Cha Mapinduzi kuwa makamu mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa mwaka wa Fedha 2017/2018

Kuunda kamati mbalimbali za Halmashauri kwa mwaka 2017/2018

KAMATI YA FEDHA,UONGOZI NA MIPANGO

1. Yohana P.Mshita Mwenyekiti wa Halmashauri
2. Saidi R.Ndiyunze Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri
3. Ezekiel M.Kabonge Mwenyekiti kamati ya Uchumi
4. Fabiano D.Doragi Mwenyekiti kamati ya huduma
5. Anna T.Mwanadota
6. Hamenyimana C.Gutabaga
7. Monika Mayoba
8. Fredrick Nyamwombo

KAMATI YA UCHUMI,UJENZI NA MAZINGIRA

1. Ezekiel M.Kabonge
2. Renatha L.Mizungo
3. Jonas Abel Kaja
4. Hilda Lusaka
5. Asia Kasebo
6. Belisia Solomon
7. Poteza L.Kilali
8. Amando A.Ndondeye
9. Moris F.Changuvu
10. Schola Thomas
11. Rebeka Dangudangu

Msimamizi wa uchaguzi alitoa maelekezo kuwa kila kamati itachagua mwenyekiti wake,hivyo wagombea nafasi ya mwenyekiti wa kamati Vyama viwili vilisimamisha wagombea kama wanavyoonekana kwenye jedwali;-

Na	Jina Kamili	Chama
1	Ezekiel M.Kabonge	CCM
2	Poteza L.Kilali	NCCR MAGEUZI

Jumla ya wajumbe waliopiga kura walikuwa 11 hakuna kura iliyoharibika.Baada ya kuhesabu kura matokeo yalikuwa kama ifuatavyo;-

Na	Jina Kamili	Chama	Idadi ya Kura
1	Ezekiel M.Kabonge	CCM	8
2	Poteza L.Kilali	NCCR MAGEUZI	3
			11

Msimamizi wa uchaguzi alimtangaza Mheshimiwa **Ezekiel M.Kabonge** kutoka Chama Cha Mapinduzi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira kwa mwaka wa Fedha 2017/2018

KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII

1. Fabiano D.Doragi
2. William Luturi
3. Baraka Mkuyu
4. Goddy Nkulizo
5. Eliya Kagoma
6. Banka Balagulana
7. Mbiha N.Issaya
8. Elias Masende
9. Fidel Mtemwa
10. Agnes Kanyamangenge
11. Mwasi Mchunga

Msimamizi wa uchaguzi alitoa maelekezo kuwa kila kamati itachagua mwenyekiti wake,hivyo wagombea nafasi ya mwenyekiti wa kamati Vyama viwili vilisimamisha wagombea kama wanavyoonekana kwenye jedwali;-

Na	Jina Kamili	Chama
1	Fabiano D.Doragi	CCM
2	Eliya C.Kagoma	NCCR MAGEUZI

Jumla ya wajumbe waliopiga kura walikuwa 12 hakuna kura iliyoharibika.Baada ya kuhesabu kura matokeo yalikuwa kama ifuatavyo;-

Na	Jina Kamili	Chama	Idadi ya Kura
1	Fabiano D.Doragi	CCM	8
2	Eliya C.Kagoma	NCCR MAGEUZI	4
			12

Msimamizi wa uchaguzi alimtangaza Mheshimiwa **Fabiano D.Doragi** kutoka Chama Cha Mapinduzi kuwa mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira kwa mwaka wa Fedha 2017/2018.

KAMATI YA MAADILI

1. Hamenyimana C Gutabaga Mwenyekiti
2. Jonas Abel Kaja Mjumbe
3. Elias Masende Mjumbe

KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

1. Saidi R.Ndiyunze Mwenyekiti
2. Beilisia Solomon Mjumbe
3. Mbiha Issaya Mjumbe
4. Fidel Mtemwa Mjumbe

AJIRA

1. Sabas C.Matabura.

ALAT

1. Agnes Kanyamangenge
1. Goddy Nkulizo

ARDHI

1. Hilda Lusaka
2. Rebeka Dangudangu

HWK/BM/AG/NA/26/2016/2017 KUPITISHA RATIBA YA VIKAO VYA HALMASHAURI KWA MWAKA 2017/2018,

Ratiba ya vikao vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2017/2018 iliwasilishwa mkutanoni na kupitishwa ili itumike kwa mwaka 2017/2018.

Wajumbe walisisitiza kuwa Ratiba ya vikao vya Halmashauri kwa mwaka 2017/2018 ifuatwe.Pia walisisitiza wawe wanapewa taarifa kuhusiana na mabadiliko ya Ratiba za Vikao hususani zinapotokea dharura zisizo zuilika.